NADHARIA ZA TAFSIRI, UKALIMANI NA UUNDAJI WA ISTILAHI



Mhariri
Hadija Jilala

Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa istilahi ni kitabu kilichoandikwa ili kuenzi mchango wa Profesa Hermas J. M. Mwansoko katika taaluma ya tafsiri, ukalimani, uundaji wa istilahi na maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Kitabu hiki kina sura zilizoandikwa na wanazuoni waliobobea katika uga wa tafsiri, ukalimani, uundaji wa istilahi na lugha ya Kiswahili kutoka katika vyuo vikuu mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kwa hiyo, ni kitabu chenye hadhi ya kimataifa kilichosheheni mawazo ya kinadharia na vitendo kuhusu tafsiri kutoka katika muktadha wa kimataifa. Kwa ujumla, kitabu hiki kimezitalii na kuziangazia taaluma za tafsiri, ukalimani, uundaji wa istilahi na maendeleo ya lugha ya Kiswahili kwa ujumla. Ni kitabu ambacho kinaziba pengo la uhaba wa vitabu vya nadharia za tafsiri katika Kiswahili na kutoa mwongozo na maarifa ya kinadharia na vitendo kuhusu tafsiri, ukalimani na uundaji wa istilahi. Kwa maana hiyo, tunategemea kuwa wanafunzi, walimu, watafiti, wafasiri, wakalimani na wapenzi wa taaluma hizi watafaidika na kitabu hiki ambacho kimekuja katika wakati mwafaka.

Mhariri wa kitabu hiki Dkt. Hadija Jilala, ni mwanazuoni aliyebobea katika fani ya tafsiri. Amefanya kazi kadhaa za tafsiri za kitaifa na kimataifa. Amefanya tafiti na kuandika makala katika uga wa tafsiri na utamaduni. Mpaka sasa ni Mhadhiri wa tafsiri na taaluma za Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mwandishi wa dibaji ya kitabu hiki, Prof. Daniel. J. Mkude, ni Profesa wa isimu ya Kiswahili katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia ni mbobezi katika uga wa Tafsiri. Katika uga huu, amefanya tafiti na kusimamia tafiti pevu zaidi zilizozalisha PhD za kwanza katika fani hii nchini Tanzania wanafunzi wake wakiwa ni Dkt. Pendo Malangwa (2010) na Dkt. Hadija Jilala (2014). Kwa hiyo, huwezi kuzungumzia tafsiri nchini Tanzania bila kumtaja Pofesa Daniel Mkude.

DAUD PUBLISHING
Company Limited

YALIYOMO

DIBAJI vi
UTANGULIZI vi
SHUKRANI xxi

SEHEMU YA KWANZA 1
NADHARIA ZA TAFSIRI, MBINU NA VITENDO 1

Sura ya Kwanza 2
Ukuzaji wa Kiswahili Kupitia Tafsiri: Hatua Moja Mbele, Mbili Nyuma 2
Hermas J. M. Mwansoko 2
Sura ya Pili 19
Nadharia za Tafsiri na Ukalimani 19
Titus Mpemba 19
Sura ya Tatu 52
Uhakiki wa Nadharia za Tafsiri 52
Mosol Kandagor na *Salim K. Sawe* 52
Sura ya Nne 70
Uhakiki wa Nadharia ya Skopos katika Tafsiri: Mifano ya Tafsiri ya Matini za Kiutamaduni 70
Hadija Jilala 70
Sura ya Tano 92
Tathmini ya Utumizi wa Mbinu za Newmark (1988) katika Kutafsiri Matini za Kiutamaduni 92
Hadija Jilala 92
Sura ya Sita 114
Ulinganifu katika Tafsiri: Suluhisho kutoka kwa Isimu Tendaji 114
Nahashon A. Nyangeri na Enock Matundura 114
Sura ya Saba 130
Ubinafsishaji wa Tovuti kwa Kiswahili na Maendeleo 130
Vincent N. Magugu, Robert W. Oduori na *Sarah Marjie-Okyere* 130
Sura ya Nane 149
Tafsiri za Vivumishi Vitumiavyo Kiunganishi "Kama" 149
Nelli V. Gromova 149
Sura ya Tisa 157

Uchambuzi wa Masuala ya Usaguzi wa Kijinsia katika Nadharia ya Tafsiri na Vitendo 157
Pendo Salu Malangwa 157
Sura ya Kumi 168
Ubinafsishaji wa Dhana Kupitia Tafsiri: Uchanganuzi wa Lugha katika Rununu ya Nokia 168
Sarah Marjie-Okyer, Robert W. Oduori, na *Vincent N. Magugu* 168

Sura ya Kumi na Moja 184
Nafasi ya Tafsiri katika Leksikografia Thaniya 184
Benard Odoyo Okal 184
Sura ya Kumi na Mbili 210
Tafsiri na Maendeleo ya Utafiti Wa Kiswahili Nchini Kenya 210
Carren Nyandiba 210

SEHEMU YA PILI 221
NADHARIA ZA TAFSIRI KATIKA FASIHI 221

Sura ya Kumi na Tatu 222
Uchambuzi wa Nadharia ya Ulinganifu katika Fasihi 222
Hadija Jilala 222
Sura ya Kumi na Nne 245
Nadharia ya Mifumo Mingi: Suluhisho la Matatizo ya Tafsiri za Kifasihi 245
Rehema Stephano 245
Sura ya Kumi na Tano 256
Tenzi Tafsiriwa katika Kiswahili: Ruwaza ya Shujaa Inavyojenga Falsafa katika Utenzi wa Kalevala 256
Asifiwe Mwagike na *Shani Omari* 256
Sura ya Kumi na Sita 279
Visawe katika Methali Tafsiriwa za Kiswahili 279
Joseph Nyehita Maitaria na *Clara Momanyi* 279
Sura ya Kumi na Saba 294
Tafsiri katika Tamthiliya ya Kuigizwa 294
Nasra Habibu 294
Sura ya Kumi na Nane 308
Tafsiri ya Mandhari na Jazanda katika Tawasifu ya Unbowed, A Memoir

Elizabeth Ombito Khalili 308

SEHEMU YA TATU 324
NADHARIA ZA UKALIMANI 324
Sura ya Kumi na Tisa 325
Ukalimani: Kichocheo cha Kuhama toka Ujima hadi Utandawazi, Sayansi na Teknolojia 325
Mnata Resani 325

Sura ya Ishirini 345
Changamoto za Ukalimani katika Maendeleo ya Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka Kibonzo cha Kirikou 345
Pendo Mwashota na *Neema Amos Chaula* 345
SEHEMU YA NNE 356
UUNDAJI WA ISTILAHI 356
Sura ya Ishirini na Moja 357
How did Bantu Language Speakers come up with a Word for "Food"? 357
Herman. M. Batibo 357
Sura ya Ishirini na Mbili 369
Changamoto za Kutafsiri Matini za Ushauri Nasaha Jamii: Faida ya Uundaji wa Faharasa 369
Ahmad Kipacha 369
Sura ya Ishirini na Tatu 389
Ufinyazaji kama Mbinu ya Uundaji Msamiati katika Kiswahili 389
Godian Katikiro 389
Sura ya Ishirini na Nne 406
Mchango wa Prof. Hermas J. M. Mwansoko katika Uundaji wa Istilahi na Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili 406
Ahmed Y. Sovu 406

SEHEMU YA TANO 419
TAFSRI KATIKA ELIMU 419
Sura ya Ishirini na Tano 420
Dhima ya Tafsiri katika Ufundishaji wa Lugha ya Kigeni/Pili: Mfano Lugha ya Kiswahili 420
Zabroni T. Philipo 420
Sura ya Ishirini na Sita 438

Changamoto za Ufundishaji wa Mada ya Tafsiri na Ukalimani katika Shule za Sekondari Tanzania Bara 438
Leonard H. Bakize 438

SEHEMU YA SITA 452
MAENDELEO YA LUGHA NA FASIHI YAKE 452
Sura ya Ishirini na Saba 453
Utandawazi wa Lugha za Kiafrika: Nafasi ya Kiswahili Sanifu katika Afrika Inayobadilika 453
Aldin K. Mutembei 453
Sura ya Ishirini na Nane 477
Tathmini ya Utekelezaji wa Matamko ya Viongozi Waandamizi wa Serikali ya Tanzania kuhusu Matumizi ya Kiswahili 477
Mussa M. Hans 477

TAARIFA KUHUSU WAANDISHI 497

Sura ya Ishirini na Nane

Tathmini ya Utekelezaji wa Matamko ya Viongozi Waandamizi wa Serikali ya Tanzania kuhusu Matumizi ya Kiswahili

Mussa M. Hans

Utangulizi

Matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini Tanzania yana historia ndefu kwa kuwa ndio lugha pekee iliyotumika kuwaunganisha wananchi katika harakati za kudai uhuru. Mara baada ya kupata uhuru, viongozi wa serikali ya Kizalendo wakaendelea kuenzi matumizi ya Kiswahili kwa namna mbalimbali. Mathalani, mwaka mmoja tu mara baada ya nchi ya Tanganyika kupata uhuru, rais wa kwanza wa Tanganyika mwalimu Julius Nyerere alilihutubia Bunge kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hii ilikuwa ni hatua muhimu sana katika historia ya maendeleo ya lugha hii hasa ikizingatiwa kwamba ilifanywa na mtu mwenye mamlaka makubwa serikalini, na zaidi ya yote alilifanya jambo hilo katika chombo chenye mamlaka makubwa ya kisheria na ambacho kina uwakilishi wa wananchi wote.